# MUNGU PEKEE WA KWELI

Shauku kuu ya mwanadamu ni kuishi maisha marefu. Kila mmoja anaogopa kifo; naam, anatamani laiti angeishi milele na asipatwe na mauti kamwe. Je jambo hili linawezekana?

Takribani miaka elfu mbili iliyopita, Mungu wa mbinguni alimtuma mjumbe wake, Yesu Kristo. Ujumbe aliouleta kwa wanadamu wote ulikuwa hasa ni kuhusiana na namna ya kuepukana na mauti na kuishi milele. Alisema hivi kuhusu ujumbe wake; ***"kama vile ulivyompa mamlaka juu ya wote wenye mwili, ili kwamba wote uliompa awape uzima wa milele" Yohana 17:2.***

Kwa hivyo ni wazi kwamba injili ya Yesu Kristo inahusu jinsi gani mwanadamu anaweza kuishi milele. Sasa je! Ni kwa jinsi gani hili litafanyika? Sikia kile asemacho; ***"Na uzima wa milele ndio huu, Wakujue wewe, Mungu wa pekee wa kweli, na Yesu Kristo uliyemtuma" Yohana 17:3.***

Naam; ili tuweze kuepuka mauti; ili tuishi maisha yasiyo na ukomo milele; basi ni lazima iwe ni kwa njia ya kumjua Mungu pekee wa kweli. Na hii inatuleta kwenye mada yetu tunayoianza kwa swali kama ifuatavyo;

## MUNGU NI NANI?

Hebu na tuyaangaliye yote yale yatuzungukayo. Tunaona nini? Kuna miti ya aina mbali mbali. Tunaona wanyama, wadudu na ndege wa aina mbali mbali. Kuna bahari kubwa yenye maelfu ya aina mbali mbali ya viumbe ndani yake. Sasa je! vyote hivi vimetoka wapi? Ni nani aliyevifanya vikawepo?

Wanadamu katika utafiti wao wa kisayansi waligundua kwamba uhai *{maisha}* unaweza kutoka ama kutokana na uhai mwingini; yaani uhai unatokana na uhai. Na tena waligundua kwamba, kila matokeo yana sababu zake. Kwa hivyo basi; ni nani aliyevifanya vitu hivi vyote tuvionavyo vikituzunguka?

Watu wakuu wameishi katika dunia hii. Tunasoma na kusikia kuhusu wafalme wakuu walioitawala dunia yote. Na kuhusu pia watu wenye hekima waliofanya mavumbuzi makubwa. Lakini je! tumesikia hata mmoja wao akidai kuwa ndiye aliyevifanya *{aliyeviumba}* vyote hivi tuvionavyo? Je! tunamfahamu mwanadamu aliyefanya ama kusababisha uwepo wa viumbe vituzungukavyo? Sote tunakubaliana kwamba hakuna madai kama hayo miongoni mwa wanadamu. Sasa basi; ikiwa uhai ni lazima utokane na uhai, na matokeo lazima yawe na sababu zake; ni nani aliyeleta uhai na uwepo wa vyote hivi?

## MUNGU NI MUUMBAJI

Ujumbe wa Mungu kupitia kwa manabii unatuambia kwamba, ***"yuko Mungu mbinguni afunuaye siri" Danieli 2:28.*** Kwa hivyo ni huyo Mungu ndiye aliyevifanya vitu vyote, vionekanavyo na visivyoonekana; maana mjumbe anatuambia kwamba; ***"Hapo mwanzo Mungu aliziumba mbingu na nchi" Mwanzo 1:1.*** Anaendelea kulithibitisha hili akisema; ***"Wewe ndiwe BWANA, wewe peke yako; wewe ulifanya mbingu, mbingu za mbingu, pamoja na jeshi lake lote, dunia na vyote vilivyomo, bahari na vitu vyote vilivyomo, nawe unavihifadhi vitu hivi vyote…" Nehemia 9:6.***

Huyu Mungu anathibitisha uumbaji wake akisema; ***"Mtanifananisha na nani, basi, nipate kuwa sawa naye?...Inueni macho yenu juu, mkaone; ni nani aliyeziumba hizi; aletaye nje jeshi lao kwa hesabu; aziita zote kwa majina; kwa ukuu wa uweza wake, na kwa kuwa yeye ni hodari kwa nguvu zake; hapana moja isiyokuwapo mahali pake…Yeye ndiye anayeketi juu ya duara ya dunia, na hao wanaokaa ndani yake huwa kama panzi; yeye ndiye azitandazaye mbingu kama pazia na kuzikunjua kama hema ya kukaliwa" Isaya 40:25-26,22;*** *soma pia* ***Zaburi 104.*** Kwa hivyo baada ya maelezo haya yote, kwa ujasiri tunaweza kujibu swali letu kwamba, Mungu pekee wa kweli ndiye muumbaji wa vitu vyote, na mwenye kuudumisha uwepo wao. Hii ndiyo maana maisha yasiyo na ukomo *{yaani uzima milele}* yanaweza kufikiwa tu kwa kumfahamu yeye vyema; maana tukimfahamu yeye; basi tutayafahamu maisha ambayo tuliumbwa ili tuishi kwayo. Kwa hivyo je! Mungu ni muumbaji? Lakini mtu anaweza kushangaa na kuuliza zaidi kwamba, huyu Mungu muumbaji ni nani ama ni nini?

## MUNGU NI FAMILIA

Tunaona makaburi ya mawe; mengine yakiitwa miti mitakatifu ya mababu, sanamu ya Yesu, Mariamu na wengineo zikiitwa takatifu. Je! Mungu muumbaji yuko katika vitu hivi? Je! anajitambulisha kwa njia hizi? Hebu twende kwa mjumbe naye atatuambia, maana yeye peke yake ndiye ajuaye, kwani alikuwako kwa Mungu. Hebu mtu ye yote asiwadanganye, maana anatuambia kwamba; ***"wala hakuna amjuaye Mwana ila Baba; wala hakuna amjuaye Baba ila Mwana, na ye yote ambaye Mwana apenda kumfunulia" Luka 10:22.***

Tukiwa na hayo akilini mwetu, hebu sasa tumsikie mjumbe kwamba anasema kuwa Mungu ni nani/nini. Ili tuweze kufahamu, tunapaswa kurudi nyuma ambapo vyote vilianzia, naam; pindi ambapo Mungu alikuwa hajaanza kuumba. Anatuambia; ***"Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu" Yohana 1:1.*** Wakati huo uumbaji wa ***Mwanzo 1:1*** ulikuwa haujaanza bado. Alikuwapo Mungu peke yake. Na alikuwa bado hajaanza kuumba. Sasa je! tunaona nini hapa?

## MUNGU SI UTATU

Tumesikia mafundisho yanayomwonesha Mungu kuwa ni utatu *{yaani nafsi tatu ndani ya mmoja ama mmoja mwenye nafsi tatu}*. Lakini kwa kufuata maelekezo aliyompa Kristo kutuletea, tunaona kitu kilicho tofauti kabisa. Hebu turudi nyuma katika fungu tafadhalini. ***"Hapo mwanzo alikuwako Neno".*** Huyu ni nafsi kamili inayojitegemea – Neno. Hebu twendelee pamoja. ***"Naye Neno alikuwako kwa Mungu".*** Alikuwako kwa Mungu ambaye pia ni nafsi nyingine inayojitegemea – huyu ni nafsi nyingine tofauti na Neno. Watu wengi hawalielewi hili na hivyo kuyafasiri ama kuyaelezea Maandiko vibaya. Hapa imetumika lugha rahisi na ya wazi kabisa. Kuwa pamoja na mtu mwingine, ni lazima muwe nafsi mbili zilizo tofauti, na si ndani ya mwingine.

Kwa hivyo hapo mwanzo, Mungu na Neno *{yaani wawili}* walikuwa pamoja. Hapa tunawaona wawili *{yaani nafsi mbili tofauti}* na si watatu. Na kwa sababu hiyo; fundisho la utatu ni la uongo.

Hebu twendelee na fungu letu ili tuone utata na kutokuelewa kwa watu kunatokana na nini. ***"Naye Neno alikuwa Mungu".*** Inakuaje Neno awe pamoja na Mungu na kwa wakati huo huo awe Mungu?

## MUNGU – JINA LA FAMILIA

Ukweli ni kwamba; Mungu ni familia ya uumbaji yenye nafsi mbili zinazotumia jina moja. Neno ***{Yohana 1:1}*** alikuwa BWANA Mungu aliyewaumba Adamu na Hawa; aliyenena na Nuhu, Ibrahimu, Musa na Manabii wote; na ndiye ambaye baadaye alivaa mwili wa kibinadamu na kufanyika *{akawa}* Yesu Kristo ***{soma Mwanzo 2:7; Kutoka 3:4-5; Zaburi 18:2; Isaya 43:13; Yohana 1:14; 8:28; 1 Wakorintho 10:4; 1 Petro 1:10-11}.*** Tafadhali soma mafungu haya katika biblia yako kwa mfululizo uliowekwa hapa.

Nafsi nyingine ni Mungu ambaye Neno *{yaani Yesu}* anamwelezea kama Baba, na kuhusiana naye anasema; ***"Hakuna mtu aliyemwona Mungu wakati wo wote; Mungu Mwana*** *{Yesu}* ***pekee…huyu ndiye aliyemfunua*** *{ama aliyemtambulisha}****".*** Na tena; ***"Sauti yake hamkuisikia wakati wo wote, wala sura yake hamkuiona" Yohana 1:18; 5:37.***

Ikiwa si nafsi zilizo tofauti; basi Yesu asingeweza kuwaambia wanadamu kwamba hakuna mtu aliyemwona Baba wala kuisikia sauti yake wakati kabla ya ujio wake, manabii waliongea na Mungu. Aliyasema hayo akiwa miongoni mwa wanadamu. Kwa hivyo; ni hawa wawili *{na si watatu}* ndio waliokuwapo tangu mwanzo na huku wakishiriki jina moja, yaani Mungu, likiwa jina la familia yao. Ni hii familia ya wawili ndiyo iliyosema; ***"Mungu*** *{familia moja}* ***akasema, Na tumfanye*** *{sisi wawili}* ***mtu kwa mfano wetu…" Mwanzo 1:26.***

Kwa hivyo basi; elewa na fahamu kwamba Mungu ni mmoja *{kwa maana ya familia moja},* familia yenye nafsi mbili ama wana familia wawili. Hii ndiyo sababu, Yesu Kristo katika kipindi chote cha maisha yake ya kimwili alikuwa akizungumza kuhusu yeye mwenyewe pamoja na Baba, yaani wawili tu ***{soma Yohana 5:17,19-23,30,37,43; 6:40,44,57; 10:17-18,30; 12:49-50; 13:1; 14:16,23,28; 17; 1 Yohana 1:2-3 n.k}.***

## ROHO MTAKATIFU

Ukichukua panga ukakata mti na kuuangusha chini; je! unasema ni nguvu zako ndizo zilizofanya hivyo? Bila shaka. Je! waweza kuuzungumzia uwezo *{nguvu}* wako wa kupanga na kutenda mambo kama nafsi nyingine ndani yako? Hapana! Kadhalika na kwa Mungu pia. Familia ya uumbaji ya Mungu ni roho ***{Yohana 4:24},*** isiyoweza kuonekana kwa macho yetu ya kimwili. Kwa hivyo atendapo mambo; basi kile tukionacho sisi ni matokeo tu. Ile nguvu aitumiayo ndiyo ambayo sisi tunaiita Roho Mtakatifu; maana anasema, ***"Waipeleka roho yako, wanaumbwa, Nawe waufanya upya uso wa nchi" Zaburi 104:30.*** Naam; kila wakati atakapo kufanya lo lote, nguvu aitumiayo ni roho takatifu. Wakati alipoufanya upya uso wa nchi *{yaani dunia; Mwanzo 1:3-31},* ***"Roho*** *{uwezo/nguvu}* ***ya Mungu ilitulia juu ya uso wa maji" Mwanzo 1:2.***

Aliamuru na vitu vikafanyika, lakini anasema; ***"mkono wangu umeuweka msingi wa dunia, na mkono wangu wa kuume umezitanda mbingu, niziitapo husimama pamoja" Isaya 48:13.*** Hapa anasema ni mkono wake ndio ulioumba, na mkono wake katika fungu tulilosoma ni roho aliyoipeleka na vitu vikaumbwa ***{Zaburi 104:30}.***

Kwa hivyo basi; ni dhahiri na wazi kabisa hapa kwamba roho mtakatifu si nafsi nyingine ndani ya familia ya Mungu, bali ni uwezo *{nguvu}* wao wa utendaji; naam, ni maisha yao. Kufikia hapa; dhana ya utatu imejikwaa na kuanguka chini huku ikithibitishwa na Maandiko kuwa ni ya uongo, ni mafundisho na mapokeo ya wanadamu tu.

Hebu tuthibitishe zaidi. Kristo anasema; ***"kama vile Baba alivyo na uzima nafsini mwake…" Yohana 5:26.*** Huu uzima ni roho iwafanyayo kuwa mmoja; kwa maana ya kushiriki nia moja inayowafanya kufikiri, kunena na kutenda mamoja. Wakati mtu apokeapo roho ya Mungu *{si roho na Mungu}* inamuwezesha kufahamu, kufikiri, kunena na kutenda kama Yeye; ikitufanya kuwa mmoja na Baba na Mwana. Kwa maana anasema tumepokea ***"Roho atokaye kwa Mungu, makusudi tupate kuyajua tuliyokirimiwa na Mungu…sisi tunayo nia ya Kristo" 1 Wakorintho 2:12,16.*** Kwa hivyo, Roho Mtakatifu ni maisha, akili *{nia}* na uwezo/nguvu ya Mungu, na wala si Mungu mwingine *{si nafsi nyingine}.*

## WANAOWEZA KUWA MIUNGU

Wewe ni nani na ni kwa nini upo? Wasomi wa ulimwengu huu wamefundisha kwamba wanadamu ni wanyama, na hivyo wanaitwa mamalia. Lakini je! wako sahihi? Je! Mungu muumbaji yeye anasemaje? Sikilizeni tafadhalini.

Mungu akaumba ***"kiumbe hai kwa jinsi zake, mnyama wa kufungwa, na kitambaacho, na wanyama wa mwitu kwa jinsi zake…" Mwanzo 1:24-25.*** Hapa Mungu anatueleza wazi jinsi alivyoumba kila kiumbe hai kwa jinsi zake. Lakini kwa habari za mwanadamu anasema; ***"Na tumfanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu*** *{kwa jinsi yetu}****…" Mwanzo 1:26.*** Umeipata hiyo pointi? Mungu hakusema; *"Na tumfanye mtu kwa jinsi zake".* Bali alisema; *"Na tumfanye mtu kwa jinsi yetu, kwa mfano na sura yetu".* Tupo hapo wapendwa? Wewe na mimi tumeumbwa kwa jinsi ya Mungu; kumaanisha kwamba sisi ni wa jamii ya Mungu, na wala si wa namna nyingineyo, wala aina fulani ya wanyama!

Ikiwa sisi ni washirika wa familia ya Mungu; ni kwa nini basi sisi si viumbe wa kiroho kama Mungu alivyo? Ni kwa nini sisi ni wa kimwili huku Mungu ni wa kiroho?

## KUZALIWA UPYA

Mungu yuko hivyo alivyo kwa sababu alichagua mwenyewe kwa hiari kuwa hivyo. Kwa kuwa alimuumba mwanadamu ili awe kama yeye, basi mwanadamu anapaswa achague kwa hiari yake mwenyewe kuwa kama Mungu. Hata ingawa Mungu anataka mwanadamu aliye kama yeye, alimpa kwanza nafasi ya kuchagua mwenyewe. Nafasi hiyo ni maisha haya ya kimwili tuliyonayo sasa. Sikilizeni asemacho kuhusiana nasi sasa. ***"Mwanadamu ni nani hata umkumbuke, Ama mwana wa binadamu, hata umwangalie? Umemfanya mdogo punde kuliko malaika…" Waebrania 2:6-7.***

Kwa hivi sasa tu wadogo *{wa kiwango cha chini}* kuliko malaika kwa sababu wao ni viumbe wa kiroho huku sisi ni viumbe wa kimwili. Ni kwa nini mpangilio *{utaratibu}* huu? Ni

kwa ajili ya ujenzi *{ukuzaji}* wa tabia. Tuko katika mwili huu kwa ajili ya mafunzo.Tunahitaji kukuza *{kujifunza}* akili *{nia}* na tabia ya Mungu ndani yetu.

Adamu alidanganywa na Shetani na kwenda mbali *{kando}* na kusudi hili. Alijifunza *{alikuza}* akili *{nia}* na tabia ya Shetani *{agiza jarida letu lisemalo,* ***"JE! WEWE NI MKRISTO?"*** *kwa maelezo zaidi; nasi tutakutumia bure ujumbe huo}.*

Wakati alipokuja Yesu ambaye ni mleta amani, aliikataa akili na tabia ya Shetani na akachagua njia ya Mungu. Kwa kumwelekea Mungu, basi Mungu aliweka akili *{roho takatifu}* yake ndani yake ambayo kwayo, Kristo alichukuliwa mimba, maana anatuambia; ***"Mimi leo nimekuzaa".*** Na Mungu akawa ***"Baba yake huku Kristo akiwa Mwanawe" Waebrania 1:15.*** Katika maisha yake ya kimwili kama sisi, Kristo alifanywa mdogo kuliko malaika ***{Waebrania 2:9}.***

Kwa kuendelea kumpinga Shetani, na kumtii Mungu kwa uwezo wa roho mtakatifu, kupitia kwa mapingamizi ya Shetani, Kristo alikuza *{alijenga}* tabia ya Mungu ndani yake ***{Waebrania 5:8-9}.*** Baada ya kuwa mtiifu hata mauti, Mungu alimfufua na kumpa mwili wa roho, na kufikia hatua hiyo, alizaliwa tena, maana imeandikwa; ***"na kudhihirishwa kwa uweza kuwa Mwana wa Mungu, kwa jinsi ya roho ya utakatifu, kwa ufufuo wa wafu…" Warumi 1:4.***

Kuzaliwa kwake mara ya kwanza na Mariamu ni kuzaliwa kimwili na alikuwa mwana wa Daudi ***{Warumi 1:3}.*** Na kuzaliwa kwake mara ya pili ni kuzaliwa kiroho na akawa mwana wa Mungu. Kwa huku kuzaliwa mara ya pili, ***"amevikwa taji ya utukufu na heshima {Waebrania 2:9}"*** na kuwa mzaliwa wa kwanza wa Mungu.

Maisha aliyoishi katika mwili huu yalituonesha pale tupaswapo kupitia kabla hatujazaliwa mara ya pili, maana anasema; ***"tukimtazama Yesu, mwenye kuanzisha na mwenye kutimiza imani yetu" Waebrania 12:2.***

## UWEZEKANO WA WANADAMU KUWA MIUNGU

Tuko katika mwili huu kwa muda tu kama Kristo, ili kujifunza kumtii Mungu kwa uwezo wa Roho yake Takatifu, na kumpinga Shetani mpaka tupate kikamilifu nia *{akili}* na tabia ya Mungu. Kwa hivi sasa tu wadogo kuliko malaika. Kwa maana wote ambao hivi sasa wana roho takatifu, kama ilivyokuwa kwa Yesu; wamechukuliwa mimba, ila bado hawajazaliwa.

Kwa maana wote watakaofuzu vile vile kama Yesu, Mungu ataubadili mwili wao wa unyonge *{udogo}* upate kufanana na mwili wake wa utukufu ***{Wafilipi 3:21; 1 Wakorintho 15:52}.*** Wakati huo ndipo watazaliwa tena mara ya pili kuwa wana wa Mungu, wakiwa viumbe wa kiroho kama Baba yao alivyo. Kuzaliwa mara ya kwanza ni kuzaliwa kimwili na wazazi wetu wa kimwili *{kibinadamu}.* Kuzaliwa mara ya pili ni kuzaliwa kiroho na Baba yetu wa kiroho, yaani Mungu.

Mara jambo hili litakapofanyika; familia ya Mungu itapanuka kutoka washirika wawili *{yaani nafsi mbili, Baba na Mwana}* na kufikia mabilioni ya washirika. Kusudi la Kristo pia litakuwa limetimia, naam; lile kusudi la ***"kuwaleta wana wengi waufikilie utukufu" Waebrania 2:10.*** Naye atakuwa ***"mzaliwa wa kwanza miongoni mwa ndugu wengi" Warumi 8:29.***

Kwa hivyo elewa na fahamu kuwa wanadamu wote ni washirika wa familia ya Mungu, wakiwa miungu kama vile Mungu alivyo Mungu; maana anasema, ***"ninyi ni miungu" Yohana 10:34; Zaburi 82:6.***

Wapendwa; huyu ndiye Mungu pekee wa kweli; naye yupo hapa hivi sasa akijieleza na kujitambulisha kwako kwamba Yeye ni nani, kusudi la maisha ni nini, na kwamba ni kwa nini maisha yanategemea sana kumjua yeye. Sasa je! Huyu ndiye Mungu unayemfahamu wewe? Ikiwa siye; basi unamwabudu mungu mwingine ambaye hakukuumba na asiyejua lo lote kuhusu maisha; ambaye jina lake ni Shetani, mungu wa ulimwengu huu wa sasa *{kwa maelezo ya kina zaidi; agiza jarida letu lisemalo,* ***"SHETANI NI NANI"*** *ama kitabu chetu kisemacho,* ***"JE! KWELI SHETANI YUPO"*** *ili ujifunze zaidi. Pia kwa habari zaidi za mada hii ya Mungu pekee wa kweli; agiza kitabu chetu kisemacho,* ***"FAMILIA YA MUNGU"****}.* Sauti hii inawajilieni kutoka kwa Mungu mwenyewe kupitia kwa Kanisa lake; yaani Kanisa la Mungu.

Basi endapo utapenda kuisikia zaidi; tunayo masomo ya Biblia yatolewayo bure kabisa pasipo malipo, ni masomo yaliyotayarishwa ili kuwajulisheni kweli ya Neno la Mungu ili hiyo kweli iwaweke huru ***{Yohana 8:31-32}.***

Tunayo majarida yenye mada mbali mbali kama vile, NI WAPI PA KUANZIA?, JE! WEWE NI MKRISTO?, MNYAMA WA UFUNUO, THAMANI YA UKRISTO, ROHO YA SABATO ZA BWANA, KUOKOLEWA KWA NEEMA, KATIKA KUTAFUTA AMANI, JE! KRISTO AMEGAWANYIKA?, SHERIA ZA KIAFYA, HUYU NI SHETANI, KANISA LA SIKU ZA MWISHO, KATIKA MILENIA n.k.

Pia tunavyo vitabu kama vile, UFALME WA MBINGUNI, AMRI KUMI, KIFO NA KIYAMA, SIKUKUU ZA MUNGU, BIBLIA NA AFYA ZETU, MISINGI YA IMANI YA KANISA LA MUNGU, DINI ZA MITINDO n.k. Vyote hivi viko kwa ajili yako. Agiza sasa ujifunze ukweli wa Biblia uone maajabu ya kitabu hicho *{Biblia}* kinavyobadili maisha ya watu na kuwafikisha katika lengo sahihi la maisha na kusudi la Mungu kuwaumba wanadamu, kinyume kabisa na mafundisho ya kimadhehebu ya kidini na mapokeo ya wanadamu. Basi wasiliana nasi kwa anuani zetu zifuatazo;

**KANISA LA MUNGU – TANZANIA**

**Idara ya uchapaji na usambazaji – Mwanza**

Simu; +255 753 359 179, +255 688 359 179 & +255 655 659 179.

Barua pepe; Ukweliwabiblia@yahoo.com.sg

**Idara ya usambazaji;**

ARUSHA – Simu; +255 754 028 574 & +255 782 422 216.

DAR ES SALAAM – Simu; +255 762 055 056 & +255 672 611 204.

MARA – Simu; +255 755 409 202.

**KANISA LA MUNGU – KENYA**

**Idara ya uchapaji na usambazaji;**

NAIROBI – Simu; +254 739 434 639.

Barua pepe; endcog@gmail.com

**KANISA LA MUNGU – UGANDA**

**Idara ya usambazaji;**

KAMPALA – Simu; +256 754 167 854.

***Neema na iwe kwenu na amani zitokazo kwa Mungu Baba yetu na kwa Bwana wetu Yesu Kristo. Utukufu, heshima na uweza zina yeye tangu milele, sasa na hata milele; Amina.***